**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**S. L.P 880,**
**Simu: (028) 2988152,**
**Nukushi: (028) 2988153**
**Barua pepe: rbckigoma@p**
**Wavuti : www.pccb.go.tz**
**Simu ya Bure : 113**

**TAARIFA KWA UMMA**

---

**KIGOMA 28/07/2020**

# TAKUKURU (M) KIGOMA YAOKOA ZAIDI YA SHILINGI MILIONI MIA MOJA NA NNE

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi cha Aprili 2020 hadi Juni 2020, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kigoma iliendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kuzuia na kupambana na rushwa kulingana na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya Mwaka 2007.

Katika kipindi hicho TAKUKURU Mkoa wa Kigoma imefanikiwa kuokoa fedha kiasi cha shilingi 104,870,568.97. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 20,196,500/= zimeokolewa katika kazi za uchunguzi uliohusisha kutokurejeshwa kwa mikopo sugu kutoka kwa wanachama wa JIKOMBOE SACOSS iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, kulikopelekea SACOSS hiyo kushindwa kulipa akiba na amana za wastaafu pamoja na wanachama waliojitoa katika uanachama wa SACOSS hiyo.

Fedha hizo zitagawiwa leo kwa wananchi ambao ni wanachama wa SACOSS hiyo. TAKUKURU itaendelea kurejesha fedha kutoka kwa wadaiwa sugu waliobaki wasiotaka kurejesha mikopo kwa hiari.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

TAKUKURU (M) Kigoma katika kipindi cha Aprili, 2020 hadi Juni, 2020 imeendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri zote za Mkoa wa Kigoma ili kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa viwango na kwa wakati na pia kuhakikisha kwamba thamani ya fedha inapatikana. Katika kipindi hicho jumla ya miradi 11 ya sekta za Elimu, Afya na Barabara yenye thamani ya shillingi 1,163,826,023/= imefanyiwa ufuatiliaji. Katika miradi hiyo, miradi mitatu yenye thamani ya shilingi 360,136,773/= imebainika kuwa na dosari na hivyo uchunguzi umeanzishwa.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2020, TAKUKURU imepokea jumla ya malalamiko 167 ya vitendo vya rushwa na yanaendelea kufanyiwa kazi katika hatua mbalimbali. Idara zinazolalamikiwa zaidi ni pamoja na Mamlaka za serikali za mitaa (Watendaji wa kata, vijiji na mitaa), Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Kigoma, Jeshi la Polisi, na miradi mbalimbali inayotekelezwa katika Halmashuari za Mkoa wa Kigoma.

Katika kipindi hicho kesi 6 ziliendelea katika mahakama za wilaya ya Kigoma na Kasulu, zikiwemo kesi mpya tatu (3) zilizofunguliwa.

Kesi mbili (2) zilitolewa maamuzi ambapo kesi zote mbili upande wa Jamhuri ulishinda na washitakiwa kupewa adhabu na mahakama.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi tajwa TAKUKURU Mkoa wa Kigoma imeendelea kutekeleza jukumu lake la kuzuia viashiria na mianya ya rushwa katika taasisi za umma na binafsi zinazolalamikiwa. TAKUKURU imefanya Ufuatiliaji wa Maazimio ya kuziba mianya ya rushwa katika ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ambapo mapungufu mbalimbali yalibainika ikiwa ni pamoja na kutofanyika mikutano ya kisheria ya vijiji, usimamizi dhaifu kwa wakusanya mapato na ubadhirifu wa fedha.

Aidha katika Halmashauri ya wilaya ya Kakonko ufuatiliaji umebaini kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato kutoka wastani wa shilingi 25,569,201.73 mwezi Januari, 2020 kabala ya TAKUKURU kuanza ufuatiliaji hadi kufikia shilingi 57,060,408.54 mwezi Mei, 2020 baada ya ufuatiliaji kuanza kufanyika. Haya ni matokeo chanya ya ufuatiliaji wa TAKUKURU. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Septemba, 2020 TAKUKURU itaratibu vikao vya wadau ili kujadili utatuzi wa changamoto/ mapungufu yaliyobainika.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

TAKUKURU Mkoa wa Kigoma katika kipindi cha Aprili,2020 hadi Juni, 2020 imeelimisha jumla ya wananchi 2,366 kutoka makundi mbalimbali lengo likiwa ni kuwajengea uelewa wa madhara ya vitendo vya rushwa, ili kuwa katika nafasi ya kukemea, kufichua na kujitokeza kutoa ushahidi wa

vitendo au viashiria vya rushwa pale wanapohitajika kufanya hivyo. Makundi yaliyofikiwa ni pamoja na watumishi wa sekta za umma na binafsi, wananchi wa kawaida na wanafunzi ambao walielimishwa kuhusu athari za rushwa katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii na kutakiwa kujenga ujasiri wa kutoa taarifa dhidi ya watendaji wanaojihusisha na vitendo vya rushwa katika maeneo yao.

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Septemba, 2020 TAKUKURU itajikita katika kuelimisha jamii kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi, ufuatiliaji wa viashiria vya rushwa katika uchaguzi, kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya watu watakao jihusisha na rushwa wakati wa kura za maoni na katika kampeni za kuelekea uchaguzi Mkuu unao tarajiwa kufanyika mwezi Octoba 2020.

TAKUKURU Mkoa wa Kigoma inatoa wito kwa wananchi wote kushiriki katika mapambano dhidi ya Rushwa wakati wa uchanguzi kwa kuwaibua watoa rushwa, kukataa kujihusisha na vitendo vya rushwa kwa madhumuni ya kushawishika kumpigia mgombea kura mgombea, kukataa majengo yao kutumika kama sehemu ya kugawia fedha za rushwa, kutoa elimu kwa wengine juu ya madhara ya rushwa katika uchaguzi na kukemea vitendo vya rushwa vinavyofanyika katika maeneo yao.

Wananchi wanahimizwa kuwasiliana na ofisi za TAKUKURU Mkoa wa Kigoma, Wilaya Kasulu, Wilaya ya Kibondo, Wilaya ya Uvinza, Wilaya ya

Kakonko na Wilaya ya Buhigwe kwa Simu ya Bure 113 inayopatikana kupitia mitandao ya TTCL, AIRTEL, VODACOM, TIGO na HALOTEL.

**Kataa Rushwa, Jenga Tanzania**.

Asanteni kwa kunisikiliza

STEPHEN P. MAFIPA

**MKUU WA TAKUKURU (M) KIGOMA**